Sudan Kusini

Mwongozo wa Mwalimu

# Kiswahili 3

**Kiswahili kwa kidato cha Tatu (3)** kimeandikwa na wizara ya Elimu na Mafunzo kwa jumla, Ikishirikiana na wataalam wa lugha.

Kitabu hiki kinamwelimisha mwanafunzi kwa mazoezi na vitendo.

**Kila darasa linajumuisha Kitabu cha Mwanafunzi na Mwongozo wa Mwalimu.**

**Kila Kitabu cha mwanafunzi kinakupa:**

- Ufafanuzi mwafaka wa mtaala wa kitaifa.
- Msingi bora katika kiswahili.
- Uwasilishaji na ufafanuzi wa hoja unazotakiwa kujifunza.
- Mazoezi mwafaka yanayoonyesha jinsi Kiswahili Kinaweza kutumika katika mifano halisi maishani.
- Fursa ya ushirikiano kupitia kwa kazi ya vikundi.
- Michoro ya kusisimua.

**Masomo yote katika mfululizo huu wa msingi yalitengenezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Mkuu, Jamhuri ya Sudan Kusini.**

**Vitabu vimeundwa kutekeleza somo la shule za msingi,na wakati huo huo kuwawezesha wanafunzi na ujuzi unaofaa katika jamii ya kisasa ya kimataifa**

**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kitabu kitakachopatikana kikiuzwa kwa njia yoyote kitatawaliwa na muuzaji kuchukuliwa hatua za kisheria.**

**Funded by:**

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION quality education for all children

Sudan Kusini

Mwongozo wa Mwalimu

# Kiswahili 3

Kidato cha Tatu



**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kimefadhiliwa na:**

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION quality education for all children

# Jinsi ya kutunza kitabu chako.

**Mambo muhimu ya kuzingatia.**

1. Unaombwa kuhakikisha umenawa mikono kabla ya kukitumia kitabu chako.
2. Tumia kalamu ya rangi kuonyesha kazi iliyofanywa.Usikunje karatasi za vitabu.
3. Kitabu kikiharibika,hakikisha kinakarabatiwa kwa haraka.
4. Kuwa mwangalifu wakati unapomwazimu mwenzako kitabu.
5. Tafadhali kiweke kitabu chako mahali pakavu na pasipokuwa na unyevu.
6. Unapokipoteza kitabu chako, mjulishe mwalimu wako.

**Mambo unayokatazwa kufanya.**

1. Usiandike ndani au juu ya kitabu chako.
2. Usikate michoro iliyokitabuni.
3. Usirarue kurasa zozote kitabuni.
4. Usikiache kitabu kikiwa kimefunguliwa.
5. Usikiweke kitabu chako kwenye mkoba uliojazwa vitabu zaidi.
6. Usikitumie kitabu chako kujifunika wakati wa mvua.
7. Usikikalie kitabu chako.

Sudan Kusini

KIDATO CHA
3

# Kiswahili

*Mwongozo wa Mwalimu*

© 2018, THE REPUBLIC OF SOUTH SUDAN, MINISTRY OF GENERAL EDUCATION AND INSTRUCTION.
All rights reserved. No part of this book may be reproduced by any means graphic, electronic, mechanical, photocopying, taping, storage and retrieval system without prior written permission of the Copyright Holder.Pictures, illustrations and links to third party websites are provided in good faith, for information and education purposes only

Ilifadhiliwa na: GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION

Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.
Kimetadhiliwa na:

**KITABU HIKI HAKIRUHUSIWI KUUZWA.**

## FOREWORD

I am delighted to present to you this Teacher's Guide, which is developed by the Ministry of General Education and Instruction based on the new South Sudan National Curriculum. The National Curriculum is a learner-centered curriculum that aims to meet the needs and aspirations of the new nation. In particular, it aims to develop (a) Good citizens; (b) successful lifelong learners; (c) creative, active and productive individuals; and (d) Environmentally responsible members of our society. This textbook, like many others, has been designed to contribute to achievement of these noble aims. It has been revised thoroughly by our Subject Panels, is deemed to be fit for the purpose and has been recommended to me for approval. Therefore, I hereby grant my approval. This Teacher's Guide shall be used to facilitate learning for learners in all schools of the Republic of South Sudan, except international schools, with effect from 4th February, 2019.

I am deeply grateful to the staff of the Ministry of General Education and Instruction, especially Mr Michael Lopuke Lotyam Longolio, the Undersecretary of the Ministry, the staff of the Curriculum Development Centre, under the supervision of Mr Omot Okony Olok, the Director General for Quality Assurance and Standards, the Subject Panelists, the Curriculum Foundation (UK), under the able leadership of Dr Brian Male, for providing professional guidance throughout the process of the development of National Curriculum, school textbooks and Teachers' Guides for the Republic of South Sudan since 2013. I wish to thank UNICEF South Sudan for managing the project funded by the Global Partnership in Education so well and funding the development of the National Curriculum, the new textbooks and Teachers' Guides. I am equally grateful for the support provided by Mr Tony Calderbank, the former Country Director of the British Council, South Sudan; Sir Richard Arden, Senior Education Advisor of DfID, South Sudan. I thank Longhorn and Mountain Top publishers in Kenya for working closely with the Ministry, the Subject Panels, UNICEF and the Curriculum Foundation UK to write the new textbooks. Finally, I thank the former Ministers of Education, Hon. Joseph Ukel Abango and Hon. Dr John Gai Nyuot Yoh, for supporting me, in my role as the Undersecretary, to lead the Technical Committee to develop and complete the consultations on the new National Curriculum Framework by 29 November 2013.

The Ministry of General Education and Instruction, Republic of South Sudan, is most grateful to all these key stakeholders for their overwhelming support to the design and development of this historic South Sudan National Curriculum. This historic reform in South Sudan's education system is intended to benefit the people of South Sudan, especially the children and youth and the future generations. It shall enhance the quality of education in the country to promote peace, justice, liberty and prosperity for all. I urge all Teachers to put this textbook to good use.

May God bless South Sudan. May He help our Teachers to inspire, educate and transform the lives of all the children and youth of South Sudan.

Deng Deng Hoc Yai, (Hon.)
**Minister of General Education and Instruction, Republic of South Sudan**

# YALIYOMO

SURA YA 1: MASWALA YA KITAIFA ............................1

SURA YA 2: KILIMO ........................................................6

SURA YA 3: MITINDO YA MAVAZI YA KIAFRIKA ..15

SURA YA 4: HUDUMA ZA DHARURA ..........................22

SURA YA 5: TEKNOLOJIA............................................26

SURA YA 6: AJIRA .........................................................30

# SURA YA 1: MASWALA YA KITAIFA

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

**Sajili**

1. Mwalimu afafanue jinsi matumizi ya lugha hubadilika kulingana na mazingira.
2. Wanafunzi wataje sifa mbalimbali kuhusu sajili tofauti.
3. Wanafunzi wazungumzie umuhimu wa kuwepo kwa sajili tofauti.
4. Wanfunzi waigize sajili mbalimbali huku wakizingatia msamiati mwafaka.

Soma mazungumzo yafuatayo:

**MAJIBU**

1. Hii ni sajili ya mahakamani.
2. Mhusika wa 2 ni hakimu na wa 3 ni mshtakiwa.
3. Sifa kumi za sajili mahakamani. Sentensi fupi.
   a) Maswali mengi na majibu.
   b) Kuna mashahidi.
   c) Ina ukale mwingi.
   d) Kuna kujitetea kwa wanaolaumiwa.
   e) Maneno mengine yanaeleweka na washikadau wa mahakamani pekee.
   f) Ina ukali mwingi.
   g) Hutaja vifungu vya sheria.
   h) Hutafuta habari kwa kina.
   i) Vifungu vingine hutumia lugha ya Kilatini.
   j) Lugha ya heshima.
   k) Msamiati teule kama hakimu, mahakama, jela na kadhalika.
4. Una kosa, utafungwa kifungo, kujitetea, umeshtakiwa, unakubali makosa? Mshitakiwa, umepatikana na makosa.
5. 
   i) Mhusika wa 2 ni hakimu.
   ii) Mhusika wa 3 ni mshitakiwa.
   **iii)** Yule anarejelewa kama ‘’my friend’’ni mshtaki.

**B)** Beba! Beba! Wale wanataka uhondo waingie! Beba! Beba! Dereva kanyaga breki! Twende mama, twende mrembo,
Beba! Beba! Wachwa uchekwe!

**ZOEZI**

1. Sajili ya usafiri.
2. porojo -Wale wanataka uhondo waingie,twende mrembo, Wachwa huchekwe
3. Sifa kumi za sajili hii.
   a) Porojo nyingi.
   b) Sentensi fupi fupi.
   c) Wakati mwingine haina heshima.
   d) Ya kushawishi.
   e) Inalenga wasafiri.
   f) Inatoa maelezo ya usafiri mfano mahali,nauli na kadhalika

4. Msamiati teule **tano** wa sajili hii
   a) Matatu
   b) Abiria
   c) Dereva
   d) Usafiri
   e) Nauli
   f) Kondakta
   g) Mizigo
   h) Steni

C)

**MAJIBU**

1. Mhusika Y ni mwalimu na Z ni mwanafunzi.
2. Wahusika wako ofisini/darasani.
3. Hujambo, ninaweza kuingia, asante, pole, tafadhali
4. Mhusika Z ana heshima,ni mtiifu,ni mwaminifu-hadanganyi.
5. Sifa za sajili hii.
   a) Ni ya heshima.
   b) Hulenga mada husika.

c) Maneno ya adabu hutumika.
d) Hutumia maelezo
e) Kuna kuuliza na kujibu maswali.
f) Inatumia sheria zilitungwa
g) Msamiati wake teule ni kama mwalimu, mwanafunzi, kusoma, mtihani, vitabu.

D) Orodhesha sifa kumi za:

1. Sajili ya magazeti
   a) Hujitokeza kwenye magazeti au majarida.
   b) Muhtsari wa yaliyomo hutolewa kurasa za mwanzo.
   c) Vichwa huandikwa kwa herufi kubwa.
   d) Vichwa huwa vya kushawishi.
   e) Mitindo ya maandishi huwa mbalimbali.
   f) Habari muhimu huwa ukurasa wa kwanza na wa mwisho.
   g) Lugha ya kitaaluma hutumika.
   h) Hutumia lugha ya kuripoti.
   i) Baadhi ya Sentensi huwa fupifupi.
   j) Kuna matumuzi ya picha.
   k) Hutumia mbinu rejeshi.
   l) Kauli huwa fupi.
   m) Hueleza mambo ambayo tayari yamefanyika.
   n) Lugha ni ya wastani.

2. Sajili ya hospitali
   a) Lugha ya heshima.
   b) Imejaa maswali na maelezo.
   c) Ni ya kufariji.
   d) Ni ya upole.
   e) Maandishi yake hueleweka na wataalamu wenyewe.
   f) Ina maagizo mfano jinsi ya kutumia dawa.
   g) Ni ya matumaini.
   h) Ni yenye utafiti mwingi.
   i) Ni ya kushawishi na kujali.
   j) Msamiati teule ni daktari, dawa, mgonjwa, sindano, mochari.

## KUSOMA

### SAJILI YA DINI

**MAJIBU:**

1. Kurani, Biblia, nyimbo za injili, mahubiri
2. Lugha ya dini imebadiliki maana maandishi ya kisasa yanatumika.
3. Lugha ya kale katika dini inasaidia kuhifadhi maandishi.
4. Wanaweza kutafsiri wanachokisema kwa Kiarabu bila kupotosha waumini wao.
5. Mwandishi anaposema "Msamiati wa lugha ya kidini huwa maalum'' anamaanisha kila dini ina msamiati wake lakini misamiati tofauti inamaanisha kitu kimoja.
6. Sifa za Mungu kulingana na kifungu ni Mwenyezi, mwenye uwezo wote.
7. Mwanafunzi kulingana na dini yake, athibitishe hoja kuwa sajili ya dini hutumia lugha yenye ukali. Mwalimu hakiki majibu kwa msimamo wa imani ya mwanafunzi.
8. Undugu unajitokeza kupitia matumizi ya msamiati kama ndugu, dada, wapendwa.
9. Mwanafunzi ataje maneno ya kutasfidi anayoyajua katika sajili ya dini yake. Mwalimu hakiki majibu kwa imani ya mwanafunzi.
10. Huongozwa kwa ibada.,maombi,mahubiri,ndoa na mazishi huheshimu, matumizi ya mafumbo,taswira, methali,ina takriri au kurudiarudia, hunukuu mafungu, uzungumzaji wa kasi, mila, hadithi za mafunzo husimuliwa, sentensi fupi, maelezo ya kina, hadhira huhusishwa kwenye ibada.

## SARUFI

**VITENZI**

1. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kufafanua dhana ya vitenzi.
2. Wanafunzi wataje mifano ya vitanzi.
3. Wanafunzi watambue aina za vitenzi.
4. Wanafunzi watambulishe aina za vitenzi katika sentensi.
5. Wanafunzi wakamilishe zoezi kuhusu vitenzi katika vitabu vyao.
6. Mwalimu ahakiki majibu ya wanafunzi.

## KUANDIKA

1. Mwanafunzi andike mazungumzo baina ya mzee na kijana.
2. Mwanafunzi ataje sifa za sajili ya mchezo wa kandanda.
3. Mwanafunzi atoe sifa za sajili hii.

Kitenzi kikuu hueleza tendo lililofanywa na mtenda au alilofanyiwa mtendwa, wakati wa tendo lenyewe, hali ya tendo na kauli ya tendo hilo ilhali Vitenzi visaidizi hutangulia vitenzi vikuu katika sentensi ili kuleta maana inayokusudiwa kulingana na wakati au hali.

# SURA YA 2: KILIMO

**KILIMO MUFTI**

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kusoma shairi, kisha wanafunzi wajibu maswali kuhusu shairi.

**MAJIBU**

1. Mwandishi anajivunie kilimo bora.
2. Mshairi anatuhimiza tutumie mbolea.
3. Ubeti wa 4 unasema tusingojee bahati katika ukulima lakini tufuate hatua za ukulima.
4. Kurunzi katika ubeti wa 5 ni ukulima ulio stadi.
5. Maana ya maneno yafuatayo:
    a) Masihara-dhihaka
    b) Mufti-bora
    c) Vigezo-hatua za kufuata
    d) Dua-maombi
    e) Ajira-kazi

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

**ACHANIKAYE JUANI**

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kusoma shairi, kisha wanafunzi wajibu maswali kuhusu shairi.

**MAJIBU**

1. Maudhui ya shairi ni kujikakamua katika maisha.Analaani uzembe.
2. Mshairi anawaonya wasichana katika ubeti wa 3 wasiwe tu na urembo wa nje bali atoke aende akatafute samaki ili akirudi ale kwa ugali.
3. Ubeti wa 5 kwa lugha ya kawaida.-mkulima anaambiwa ana jembe na anajua umuhimu walo.Anaambiwa aamke akalime avune maembe na mboga kwani ana uwezo wa kulima.
4. Maana ya ‘’kipanda utachuma’’ ni kuwa ukipanda utapata mavuno.
5. Mwandishi anawalenga watu wote kwa ujumla ya kwamba wasikae bila kufanya kazi.

## KUSOMA

**Kifungu A**

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kifungu.

**KILIMO**

**MAJIBU**

1. Kilimo ni kazi ya kulima na kupanda mimea shambani.
2. Kulingana na kifungu upanzi hutegemea misimu.
3. Mashamba hutayarishwa wakati wa kiangazi.
4. Matayarisho matatu ya shamba.
    a) kufyeka,
    b) kung'oa visiki,
    c) kulima
5. Aina ya mifugo ambayo mkulima anaweza kufuga ni ng'ombe, kondoo, mbuzi, nguruwe na sungura.
6. Mimea imegawa kwa manufaa mawili.
    a) Mimea inayokuzwa kwa ajili ya chakula.
    b) Mimea ambayo hukuzwa kwa ajili ya kuuzwa.

7. Mifano mitatu ya mimea ianayokuzwa kwa ajili ya kuuzwa ni pareto, kahawa, chai na pamba.
8. Matumizi ya pareto:
    a) Pareto hutumiwa nchini kutengenezea dawa za kunyunyuzia wadudu waharibifu.
    b) Pamba: Mpamba pia hutumiwa katika viwanda vya kutengeza nguo.
9. Kilimo kimegawika mara mbili -kilimo cha ufugaji na kilimo cha chakula..
10. Sababu mbili za kufuga mifugo wachache.
    a) kupata maziwa ya matumizi yao ya kila siku
    b) kuuza ili kupata pesa za kukidhia mahitaji mengine.

11. Nyama hupatikana kutoka kwa wanyama kama ng’ombe, mbuzi, kondoo, na nguruwe.
12. Maana ya kilimo cha bustani ni upandaji wa maua na mboga.
13. Umuhimu wa kilimo cha bustani ni kuwa kimeinua uchumi wa nchi.
14. Nchi huwa dhaifu isiyoweza kutegemewa, watu hubakia kuwa wa kuombaomba kila wakati.
15. Uhaba wa kazi umesababishwa na ongezeko la idadi ya watu na pia ukuaji wa kikonokono wa uchumi wa nchi.
16. i) Kupunguza kasi ya uhamiaji mijini wa watu.
    ii) Kukabiliana na msongamano wa watu mijini.
17. Vijana wengi wanaohitimu masomo wanakabiliwa na ukosefu wa kazi na hutupwa jijini ambamo hawaambulii lolote.
18. Wananchi wengi ambao wangependa kulima hujipata wakilima visehemu vidogovidogo mno vya ardhi ambavyo haviwezi kumudu mahitaji yao
19. Kulingana na kifungu majira ya kiangazi yamekuwa marefu na makali.
20. Madhara yanaoletwa na ukosefu wa mvua-mifugo hukondeana na kuwa vifefe, chakula nacho huadimika kabisa, wananchi wa sehemu hizi hunyong’onyea na kutegemea ruzuku za chakula kutoka kwa jamii jirani na hata mataifa mengine.
21. Kwa kupanda kwenye miteremko na kutochimba mitaro ya kuzuia mmomonyoko wa udongo.
22. Kuna baadhi ya wakulima ambao wangetaka kulima lakini wanapata matatizo kadhaa.Yataje matatizo hayo
23. Ukosefu wa njia bora za usafirishaji, wakulima wadogowadogo, hupata ushindani mkubwa kutoka kwa mapapa ambao tayari wamejikita,hukabiliwa na magonjwa ambayo huua mifugo
24. Wakulima wa mboga wanakabiliwa na changamoto ya mazao yao kuweza kuharibika kutokana na ukosefu wa vyombo vya kusafirisha na gharama za juu za usafirishaji.
25. Wakulima wadogowadogo hupata ushindani mkubwa kutoka kwa mapapa ambao tayari wamejikita.
26. Waauzaji maua hukwazwa na tatizo la fedha za kulipia ushuru. Walanguzi wa maua husababishia mkulima hasara kwa kutowalipa wakulima pesa zao.

27. Kila mwananchi kuhakikisha kuwa kilimo kimepewa hadhi kinavyostahili. Vijana ambao wanakebehi kilimo hawana budi kukumbushwa kuwa ndicho uti na mgongo wanchi.
    - Maafisa wa kilimo wawatembelee wakulima nyanjani mara kwa mara ili kuwaelekeza.
    - Magonjwa ya mifugo na mimea yatafutiwe dawa
    - Barabara za mashambani ziimarishwe.

**KIFUNGU B**

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kigungu.

**MAJIBU**

1. Kulingana na kifungu unyunyiziaji wa mazao ulianza 1991.
2. njia tatu zilizotumika katika unyunyiziaji mimea maji ni
3. Mto Nile na mabaki yake na Nile Blue, Pili Mtiririko wa maji kwa mvuto, kutumia pampu.
   Mito ambayo imesaidia katika kilimo cha Sudan kusini ni mito ya Blue na White Nile.
4. Njia za unyunyiziaji maji ziliathiriwa na ukame uliotokea mnamo miaka ya 1980.
5. Sudan kusini imeamua kujiendeleza katika nyanja za utalii, makazi, fedha, kilimo.
6. Kilimo cha taifa la Sudan Kusini kilichotajika katika miaka ya 1990 ni uzalishaji wa mifugo.
7. Kilimo hiki kimeleta ajira kwa watu.
8. Uhifadhi wa mafuta unainua uchumi wa sudan Kusini.
9. Taifa la Sudan Kusini bado linategemea nchi zingine kwa ustawi wake kwa mfano mji wa Juba unapata vifaa vyake vingi kutoka Uganda.
10. Kutapunguza kukua kwa umaskini kwa kuongeza nafasi ya ajira.

**KIFUNGU C**

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kigungu.

**KILIMO CHA MPUNGA**

**MAJIBU**

1. Jamii za mijini na vijijini kupendelea zaidi kula wali na kupunguza ulaji wa vyakula vingine na kulifanya zao hili kuwa la chakula na biashara.
2. Maji husaidia mpunga kuzaa vizuri.
3. Mazingara matatu ambayo yanawezesha upandaji wa mpunga ni kilimo cha mpunga wa mabondeni, kilimo cha mpunga wa kwenye miinuko, kilimo cha mpunga cha umwagiliaji.
4. Ongezeko la miradi midogo ya umwagiliaji pamoja na matumizi ya teknolojia bora za kilimo.
5. Kufyeka, kung'oa visiki na kulima.
6. Jembe la mkono, jembe la kukokotwa na wanyama kama ng'ombe au matrekta.
7. Inarahisisha kupandikiza miche na kuhifadhi maji
8. i) Mbegu za asili ni zile ambazo zimetumika miaka mingi katika historia ya kilimo.

   ii) Mbegu zilizoboreshwa ni zile zilizoboreshwa kutokana na mbegu za asili.
9. Mbegu za asili zina ladha nzuri, uvumilivu wa matatizo mbalimbali ya kimazingira, hustahimili katika hali mbaya ya hewa na hazihitaji uangalizi wa hali ya juu.
10. Zina uwezo mdogo wa kuzaa, zinachelewa kukomaa, ni ndefu na rahisi kuanguka.
11. Huhitaji kupimwa kulingana na maelezo ya wataalamu.
12. Njia hizo ni ile ya kupanda mbegu moja kwa moja shambani na ile ya kupandikiza miche.
13. Mbegu huchukua muda wa wiki tatu hadi nne.
14. Miche hupandwa shambani kwenye mstari na kwa nafasi maalum au kupandwa kiholela bila kuzingatia nafasi maalum za kupanda.

15. Kwa sababu machipukizi huchelewa kujitokeza.
16. Kung'olea magugu kwa mkono, kwa mashine au kwa kutumia dawa ya kuua magugu.
17. Hunyonya virutubisho ardhini, yanaweza pia kuhifadhi wadudu na magonjwa yanayoweza kushambulia mimea iliyopandwa na hivyo kupunguza mavuno.
18. Umuhimu wa kupalilia mpunga ni ili kupata mavuno mengi.
19. Mpunga unanadhifishwa kwa kuurundika pahali pakavu halafu kuupigapiga ili kutenganisha masuke na mpunga.
20. Huwekwa kwenye gunia na magunia kupangwa vizuri ghalani juu ya mbao yasiguse sakafu.

**KIFUNGU D**

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kigungu.

**UFUGAJI MSETO**

**MAJIBU**

1. Ufugaji mseto ni hali ya kufuga aina mbalimbali za wanyama au miti, mboga kwa pamoja.
2. Ufugaji mseto unatokea iwapo shamba ni dogo.
3. Ni ufugaji ambao bwawa la samaki linakuwa ndani ya shamba pamoja na shughuli nyingine za shamba aidha hapo hapo shambani au katika eneo lililo mbali kidogo na shamba.
4. Kiasi anachotaka kuwekeza katika mradi,kiasi cha pesa pamoja na nguvu kazi atakayotumia kutoa huduma kwenye mabwawa ,sababu ya kufuga samaki,izingatie imani ya kidini katika eneo husika la ufugaji na walaji,suala la upatikanaji wa vyakula vya mifugo.
5. Faida sita za kufuga samaki pamoja na shughuli za shamba ni kunaongeza ufanisi, huongeza mavuno na hatimaye faida inayopatikana inakuwa kubwa. Kunakuwa na matumizi mazuri ya eneo la shamba, mazao ya kilimo ama mabaki yake hayapotei bali yanatumika katika kulishia samaki.

6. Aina tatu za ufugaji mseto wa samaki ni ufugaji mseto wa kilimo cha mazao na samaki, **m**seto wa kuku au bata na samaki, mseto wa ng'ombe, mbuzi, kondoo au sungura na samaki.
7. Mimea ni chanzo cha chakula cha samaki.
8. Kinyesi cha kuku kina virutubisho vingi kwa matumizi ya shamba pamoja na mabwawa ya samaki
9. Bata huwa wanakula viluwiluwi wa chura, vimelea vya mbu, wadudu na majani ambayo yapo ndani ya bwawa.
10. Kinyesi cha ng'ombe kina virutubisho vichache.
11. Uchaguzi wa samaki wa kufuga mseto h**utegemea mahali mbalimbali.**
12. Samaki aina ya perege anakua vizuri kama kutakuwa na mbolea za samadi na za chumvi chumvi na anaweza kuhimili kiasi kidogo cha hewa ya oksijeni. Madume ya Perege hukua haraka.
13. Samaki aina ya kambare hula vyakula vya asili ndani ya maji kama vile wadudu, konokono, vimulimuli wa chura na samaki wengine wadogo.
14. Anakua haraka sana kama chakula chenye protini kinapatikana kwa wingi, anaweza kuishi kwenye maji yenye hewa kidogo ya oksijeni, ana mifupa michache na minofu mingi, ni mtamu hasa anapokaushwa kwa moshi.
15. Hutoa mimea na wadudu wa asili ambao hutumika kama chakula cha samaki.
16. Ufugaji mseto wa samaki na mboga hulenga kuwa kitega uchumi kikubwa kwa wakulima wadogo.
17. Kwa kujenga banda juu ya bwawa kama ilivyo kwa upande wa ufugaji kuku.
18. Chakula cha bata ni kipi kwenye bwawa la samaki?
19. Mwanafunzi ataje ufugaji mseto unaondelezwa katika jamii yake. Mwalimu hakiki majibu.
20. Mwalimu hakiki majibu kulingana na msimamo wa mwanafunzi ni viluwiluwi wa chura, vimelea vya mbu, wadudu na majani ambayo yamo ndani ya bwawa.

**KIFUNGU E**

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kigungu.

**UHANDISI JENI (GMO)**

**MAJIBU**

1. Ni teknolojia ambayo hubadilisha mmea au mnyama kwa kwa njia ya teknolojia ya kuchanganya jenetiki yaani DNA (chembe hai) za mmea au mnyama mmoja na mwingine tofauti, ili kuupa mmea huo mpya au mnyama huyo mpya tabia zisizo za asili.
2. Uhandisi jeni unabadilishi mmea au mnyama kwa kuupa mmea huo mpya au mnyama huyo mpya tabia zisizo za asili.
3. Humsaidia mkulima kuvuna mazao mengi katika eneo dogo, kutotumia au kutumia kidogo dawa za kuulia wadudu na mimea kustawi vyema kwenye maeneo yenye mvua kidogo.
4. Sababu za mmea kupandwa kwenye mmea mwingine ni ili kuhamisha sifa za mmea huo.
5. Sababu inayofanya mimea iliyoko kando ya bahari kupandikizwa kwa mingine ni kuwa inafanyiwa utafiti wa kimaabara na hivyo jeni zake huchukuliwa na kuwekwa katika mimea mingine.
6. Mazao ambayo tayari yamepatikana kutokana na uhandisi jeni ni soya, pamba, canola na mahindi.
7. Nchi ambazo zimenufaika na teknolojia hii. Afrika Kusini, Burkina Faso, Misri na Sudan.
8. Wananchi wanapewe elimu ya kutosha kuhusu mazao ya GMO hasa kwa kuangalia sera, sheria, mfumo na kanuni zilizowekwa za bioteknolojia.
9. Kwa sababu ni teknolojia mpya.
10. Ilijiridhisha kuwa mazao ya chakula yaliyolimwa kwa teknolojia ya uhandisi jeni hayana madhara ukilinganisha na mazao ya kawaida.

## SARUFI

### HALI

1. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kuzungumzia dhana ya hali katika lugha ya Kiswahili.
2. Wanafunzi watofautishe kati ya hali na nyakati katika lugha ya Kiswahili.
3. Wanafunzi wavitambue viambishi vinavyoonyesha hali timilifu (me) na hali ya mazoea (hu).
4. Wanafunzi watunge sentensi kuonyesha matumizi ya hali hizi mbili.
5. Wanafunzi wakamilishe zoezi katika vitabu vyoa.
6. Mwalimu ahakiki kazi ya wanafunzi.

### Zoezi: Majibu

**Geuza sentensi zifuatazo katika hali ya mazoea.**

1. Mama hupika chakula.
2. Mtoto huandika kitabuni.
3. Wasichana huenda mtoni.
4. Mwalimu huandika kwenye ubao.
5. Sisi hulinda ng'ombe.
6. Wao hufanya mtihani.
7. Sisi thushiriki mashindano ya kandanda.
8. Seremala hutengeneza meza nzuri.
9. Wanafunzi huomba darasani.
10. Daktari humtibu mgonjwa.

## KUANDIKA

1. Mwanafunzi aandike kifungu juu ya umuhimu wa kilimo nchini mwake.
2. Mwanafunzi ajadili juu ya matumizi ya dawa za kunyunyizia mimea. Mwalimu asome insha na kuhakiki. Insha itumie mtindo wa hotuba. Hoja zilenge kilimo.

# SURA YA 3: MITINDO YA MAVAZI YA KIAFRIKA

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kulisoma shairi kabla ya kujibu maswali ya ushairi katika vitabu vyao.

**MAVAZI YA WANAWAKE**

**MAJIBU**

1. Dhamira ya mwandishi katika shairi hili ni kuonya wanawake juu ya mavazi yasiyo na heshima.
2. Mshairi analalamikia wanawake kuvaa suruali ndefu huku wakitaa utamaduni wa Mwafrika.
3. Ni mavazi yanayozungumziw katika ubeti wa 5 ni mini.
4. Mavazi yanayotajwa katika ubeti wa tano yamefanyiwa madhara ya kupasuliwa hata mpaka mapajani.
5. Madhara katika mavazi yaliyotajwa katikaubeti wa 5 yanasababisha aibu za mapaja na pia nguo za ndani kuonekana.
6. Kulingana na mshairi nia ya wanawake kuvaa siketi taiti ni kuonyesha maungo ya mwili.
7. Maana ya "Singerendi mwavalia, maziwa yanaonekana" ni kuwa wanawake wanavaa nguo zinazoonyesha matiti.
8. Wanawake mumeumbwa mkaumbika, lakini bado mnaichubua ngozi mfanane na Waarabu.Kama yangekuwa mapenzi ya Mungu ungekuwa Mwaarabu mwenye ngozi hiyo unayotamani.
9. Mtoto anaiga kile anaona mama yake akivaa.
10. Mshairi anawashauri kina mama wale wenye heshima waikemee hali ya utovu wa mavazi.

## KUSOMA

**KIFUNGU A**

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kigungu.

## MAVAZI YA KIAFRIKA

1. Mambo matatu ambayo Mwafrika alikuwa nayo kabla ya kuja kwa mzungu ni lugha, ibada na mavazi.
2. Zama za kale Waafrika walikuwa na teknolojia ya ubunifu wa hali ya juu wa kutumia mazingira yao kuweza kujitengenezea vitu mbalimbali.
3. Ulaya na Amerika.
4. Zamani Waafrika walipata vyombo vyao kutokana na mazingira.
5. Vyombo vinne ambavyo mababu wetu waliweza kujitengenezea ni zana za kilimo ,uwindaji,uvuvi, kupikia na  mavazi
6. Walitengeneza mavazi yao ya kujivika kutoka kwa ngozi za wanyama waliokuwa wakiwawinda na magome ya miti ambayo yalilainishwa na kuwa kama nguo laini.
7. Utamaduni wa Mwaafrika wa kuficha uchi ulianza na mababu zetu kwa vile walijivika maungo yao hasa sehemu za siri.
8. Kabila la Wamaasai   bado inathamini utamaduni wa kale wa mavazi.
9. Wageni kuvamia Bara la Afrikakwa ajili ya biashara na kutafuta malighafi.
10. Vitu vingine viwili tulivyovipoteza kwa wazungu na Waarabu ni ardhi na madini yetu.
11. Katika ulimwengu wa sasa mavazi ya Kiafrika yanatambulika katika matukio maalumu na katika sherehe za harusi au za kuwaaga wali.
12. Mavazi ya kisasa yanakiuka utamaduni wa Kiafrika kwa sababu watu wanavaa mavazi yasiyo na heshima yenye kuacha miili yao nje.
13. Mitindo mingi ya Kiafrika ni ya wanawake kwa sababu ndio wenye aina nyingi za mavazi.
14. Wageni wanavutiwa na mitindo mingi ya mavazi ya Kiafrika yenye rangi za kuvutia.
15. Kwa sababu mavazi haya yanaweza kukinga hali ya hewa na pia kutumika katika msimu na majira ya baridi.
16. Rangi ya hudhurungi, samawati, kijani na mchanganyiko wa rangi mbalimbali.
17. Ankara ni vitambaa ambavyo hutumia pamba kwa asilimia100% kwa hivyo unadhifu wake ni wa hali ya juu.
18. Ankara hushona vitambaa vya kichwa na jaketi

19. Vyombo vya habari vya kijamii, mazingira, teknolojia, matangazo ya biashara.
20. Waafrika waurudie utamaduni wao kwani Afrika kuna vitu vingi vizuri yakiwemo mavazi. Tuutunze na kuuenzi utamaduni wetu .

**KIFUNGU B**

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kigungu.

**SHAWISHI WA SAIZI ZERO ZA UKUBWA**

**MAJIBU**

1. Kulingana na kujenga kwa maumbo yetu ya kipekee
2. Dhana ya saizi zero inazingatia wembamba wa maumbile na kuchukulia kama urembo wa mtu.
3. Wanapata ajira katika magazeti ya mtindo.
4. Wale ambao wanazingatia sana dhana ya saizi zero ni wasichana
5. Kulingana na utafiti watoto hawafurahii ukubwa wa miili yao.
6. Watoto wanajaribu kukataa kula ili wapate saizi zero.
7. Vyombo vinazoelekezwa lawama ni magazeti, runinga na majarida.
8. Maoni yanayowapotosha watoto katika magazeti ni kwamba kupoteza uzito mwingi kutatufanya kusikia furaha.
9. Wasichana wanahitajika kuwa na mwelekeo wa maisha.Tunapaswa kufundisha wasichana tofauti kati ya picha na ukweli. Pia wasichana wanahitaji kufundishwa ujuzi wa kukataa mambo yanayoathiri umbo lao kwa vyovyote.
10. Vyombo vya habari vinapaswa kusaidia kujenga picha nzuri zaidi za mwili na sio kushinikiza watu na picha zao za umaridadi usiokuwa halisi.

**KIFUNGU C**

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kigungu.

**MADHARA YA SEKTA YA NGUO**

**MAJIBU**

1. Onyo la mwandishi kuhusu viwanda katika aya ya kwanza ni kwamba mahali kwingi kunakoshughulika na utengenezaji wa nguo, si salama.
2. Vifaa vyenye kemikali ambavyo vinatumika viwandani ni pamba, hariri, katani, kamba, na nyuzi za sasini.
3. Kupatwa na magonjwa yasiyo na tiba.
4. Viwanda vingine huwa havina vifaa vya kinga sahihi na hivyo huhatarisha usalama wa wafanyikazi, matatizo ya kurundikana pamoja, vumbi kutoka vipande vya kitambaa na rangi fulani ambayo husababishwa na kemikali yenye sumu.
5. Ng'ombe na binadamu.
6. Mchanga unaathirika kwa kuwa mabaki ya nguo yanazuia mchanga kupumua.
7. Mabaki ya nguo za nailoni yanayotupwatupwa katika mazingira yanazuia kukua kwa mimea.
8. Malipo duni, kazi nyingi za kukata pamba, kushona kwa mikono, kushonea vifungo, ajira kwa mtoto asiyefikisha umri wa kufanya kazi.
9. Wengi wa waajiriwa hawa ni vibarua wanaofanya kazi kwa masaa, siku au muda fulani.
10. Waajiri hawajali maslahi ya waajiriwa kwa vile waajiriwa wanachukuliwa kama mashine za kufanya kazi, waajiri hawatambui haki za waajiriwa wao.

**KIFUNGU D**

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kifungu.

## UMUHIMU WA MAONYESHO KATIKA SEKTA YA NGUO

### MAJIBU

1. Kulingana na aya ya kwanza, maonyesho ya nguo ni njia moja ya utangazaji wa mtindo wa mavazi mbalimbali.
2. Huchukua muda mrefu sana kutayarishwa na huhitaji utaalamu muhimu na ujuzi wa aina yake.
3. Mtazamaji anaweza kuamua kununua nguo ya aina fulani na hii ni njia ya kuinua uchumi wa yule aliyetengezaneza.
4. Maonyesho ya nguo hufanyika mara kwa mara ili kuelezea na kuwasiliana na watazamaji kuhusu mwenendo wa hivi karibuni wa mitindo.
5. Ndio, wengi hutambua ubunifu na vipaji vyao katika kubuni aina tofauti za nguo.
6. Kwa kushiriki katika maonyesho haya, wauzaji wanaweza kupata mitazamo mbalimbali ya nguo tofauti maridadi.
7. Mtengenezaji anaweze kupata ujuzi wa juu wa aina tofauti za miundo na mitindo ya nguo ili iweze kuingizwa kwenye maduka ya kibinafsi.
8. Bei nafuu ya nguo inatokea kupitia kwa picha na video za mtindo.
9. Watu wengi huchukulia maonyesho ya nguo kama njia ya kujigamba kwa wale wanaoshiriki maonyesho haya.
10. Mwandishi anawatahadharisha waigizaji wa mitindo ya nguo juu ya kudumisha heshima katika maonyesho ya mitindo ya nguo.

## SARUFI

### UKANUSHAJI WA HALI

***Hali timilifu (me) na Hali ya mazoea (hu)***

1. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kujikumbusha viambishi vinavyotumika kuashiria hali timilifu na hali ya mazoea katika lugha ya Kiswahili.
2. Kisha mwalimu awaongoze wanafunzi katika kuvitambu viambishi vya ukanushi vya hali hizi mbili.

3. Wanafunzi watunge sentensi wakikanusha hali timilifu (me) na hali ya mazoea (hu) wakitumia viambishi sahihi.
4. Wanafunzi wakamilishe zoezi katika vitabu vyao.
5. Mwalimu ahakiki majibu ya wanafunzi.

**Zoezi: Majibu**

**Kanusha sentensi hizi.**

1. Pahali hapa hapajanipendeza.
2. Mvua haijanyesha.
3. Sisi hatujakimbia sana.
4. Mama hajafua nguo.
5. Mwimbaji hajaimba vizuri.
6. Kiti hakijavinjika mguu.
7. Mti hujakatwa na mkulima.
8. Jambazi halijashikwa.
9. Wanafunzi hawajafunga shule.
10. Mtazamaji hajafaidika na maonyesho ya nguo.

**Zoezi: Majibu**

**Kanusha sentesni hizi.**

1. Daktari hawatibu wagonjwa wengi.
2. Baba hapendi kusoma gazeti.
3. Wavulana shuleni hawachezi kandanda.
4. Mwalimu hachelewi darasani.
5. Mavazi ya Kiafrika hayavutii.
6. Sisi hatulimi shambani.
7. Askari hashiki doria.
8. Yeye hatembei vizuri.
9. Darasa lao halinuki.
10. Sara hanidanganyi.

## KUANDIKA

1. Mwanafunzi aandike insha juu ya umuhimu wa mavazi ya Kiafrika. Atoe manufaa ya mavazi ya kiafrika.
2. Mwanafunzi ataje mtindo wa mavazi ya kikwao na aeleze kinachomvutia katika mtindo huo. Mwalimu ahakiki kazi ya mwanafunzi.
3. Mwanafunzi atoe msimamo wake kuhusu mavazi ya siku hizi. Insha iwe ya mjadala.
4. Mwanafunzi atoe maoni yake kuhusu kazi katika viwanda vya nguo. Mwalimu hakiki kazi ya mwanafunzi.

# SURA YA 4: HUDUMA ZA DHARURA

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kifungu.

### HUDUMA YA KWANZA

**MAJIBU**

1. Huduma ya kwanza inamaanisha huduma au msaada unaotolewa kwa mtu anayekabiliwa na ugonjwa au madhara ya ghafla.
2. La, huduma ya kwanza haitolewi kwa majeruhi wa ajali pekee pia hutolewa pia wale wamefikwa na madhara ya ghafla.
3. Umuhimu wa kisanduku cha Huduma ya Kwanza huwa na vifaa muhimu vya kuhudumia majeruhi wa ghafla.
4. Kijisanduku hiki huwa na bendeji na dawa za majeraha.
5. Wakati mtu anapopatikana baada ya ajali amejeruhiwa kwa shabaha ya kutunza uhai wake hadi daktari atakapopatikana au mjeruhiwa atakapoweza kufikishwa hospitalini. Kuzuia kuongezeka kwa madhara kwa mfano kwa kumwondoa mjeruhi sehemu yenye hatari kama moto, au hatari ya mlipuko.
6. Pigo kubwa na kitu butu.
7. Unapaswa kuangalia kwa kina na upana wa jeraha kwa mtu anayevuja damu.
8. Utatumia kipande cha nguo safi kuzuia kuvuja damu sana.
9. Kinapaswa kuwa safi sana, ili kumkinga majeruhi kutokana na kuambukizwa magonjwa mengine.
10. Kuosha jeraha na dawa Kama iodini ili kuua bakteria.
11. Sehemu mbili ambazo unaweza kumwokoa mtu kutokana na hatari ni moto na hatari ya mlipuko .
12. Katika kisa cha ajali kilichonukuliwa hapa aliyehusika kwenye ajali ni mtu mmoja-mwanamume.
13. Mambo matatu unayopaswa kufanya kabla ya kuhudumia aliyejeruhiwa pamoja na kuchukua wakati utulie kwanza, zingatia kama kuna mambo yoyote yanayokuhatarisha wewe au wengine, vile utakovyoitatua hali hii

14. Kukaribia eneo la ajali bila kujihatarisha maana barabara ina magari mengi na bado kuna magari yanayopita karibu na waathiriwa na watazamaji.
15. Walioshuhudia ajali hiyo au wale wamefika kuokoa majeruhi.
16. Kitu cha kwanza kilichoagizwa kwa ajili ya kuokoa majeruhi katika kisa hiki ni ambulensi.
17. Ili kusiwe na msongamano wa magari yaelekeze magari upande mwingine.
18. Kwa sababu huenda amejeruhiwa shingoni
19. Sababu ya wewe kutaka mtoto ashughulikiwe ni kuhakikisha hajaumia.
20. Anazua mazungumzo nao, anamhakikishia mke wa majeruhi kwamba atajua ni wapi watakapompeleka mumewe kisha amwambie iwapo yeye na mtoto wake wanaweza kuandamana naye.

**KIFUNGU B**

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kifungu.

**MAJIBU**

1. Yanaweza kusababisha maafa, uharibifu mkubwa, kupoteza mali, au athari kubwa kwa mazingira.
2. Tahadhari kabla ya tukio la mkasa kwa kusikiliza redio yako, televisheni, au taarifa na habari za dharura kutoka kwa viongozi wa umma.
3. Kuumia kwa papo hapo au hali ya matibabu ambayo inahitaji huduma ya haraka.
4. Kuna aina ngapi za dharura ya matibabu?
5. Kupoteza fahamu, ishara za mashambulizi ya moyo, ikiwa ni pamoja na maumivu makali ya kifua au shinikizo, ishara za kiharusi, ugumu kuzungumza, au kupoteza maono, kuumia kwa shingo au mgongo, mshtuko mkali au mshtuko wa umeme, uwepo wa damu katika kukohoa au kutapika, mfupa ambao umevunjika kupitia ngozi.

6. Dharura ndogo ni hali ya matibabu ambayo hahisi hatari lakini bado inahitaji huduma za matibabu kwa kipindi cha saa 24.
7. Vita, majanga ya kimaumbile, ajali, mioto na vurugu baina ya watu kama vile dhuluma za kimapenzi.
8. Kupoteza maboma yao au wapendwa wao, wanaweza pia kutenganishwa na familia au jamii zao au wanaweza kushuhudia vita, uharibifu au vifo.
9. Kuhisi kulemewa, kuchanganyikiwa au wasiweze kujua kinachofanyika. Wanaweza kuhisi woga au wasiwasi au ganzi na kujitenga.
10. Dalili hizi hutegemea hali na ukali wa matukio wanayopitia;ujuzi au tajriba yao ya matukio ya kufadhaisha yaliyopita;usaidizi walionao maishani mwao kutoka kwa wengine; afya yao ya kimwili; historia yao na ya familia yao kuhusu afya na matatizo ya kiakili;mila na tamaduni zao.
11. Ni huduma utakayowapa ni utoaji wa utunzaji halisi na usaidizi, uchunguzi wa mahitaji na matatizo, kusaidia kushughulikia mahitaji ya kimsingi, kwa mfano, chakula na maji, kuwasikiliza bila kuwalazimisha kuzungumza, kuwasaidia kutulia, kuwasaidia kupata habari, huduma na usaidizi wa kijamii, kuwalinda dhidi ya madhara.
12. Watoto na wazee, wenye matatizo ya kiakili au kikundi kilichotengwa au kilicholengwa na mkasa.
13. Baadhi yao wanalia, kushtuka, wamechanganyikiwa huku wengine wakionekana kufarijika. Wengi wao huyashuku makao haya mapya, na hawajui watakapolala, kula wala kupokea matibabu. Wengine wanaonekana kushtuka wanaposikia sauti kubwa wakifiri ni milio zaidi ya bunduki.
14. Mtoto alikuwa ameshtuka na hakuwa na wazazi au yeyote.
15. Msimulizi anazua mazungumzo ya kujali mtoto. Amfariji na kumpa matumaini.

## SARUFI

### ALAMA ZA UAKIFISHAJI

1. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kuzingumzia umuhimu wa uakifishaji katika maandishi.
2. Wanafunzi wazitaje alama za uakifishaji.

3. Wanafunzi wafafanue matumizi ya alama za uakifishaji walizo taja. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua matumizi zaidi ya alama hizo.
4. Mwalimu ataje na kufafanua matumizi ya alama za uakifishaji ambazo wanafunzi hawajataja.
5. Wanfunzi watunge sentenzi kuonyesha matumizi ya alama za uakifishaji.
6. Wamafunzi watambue utata unoweza kujiri iwapo alama za uakifishaji haztatumika ipasavyo.
7. Wanafunzi wakamilishe zoezi katika vitabu vyao.
8. Mwalimu ahakiki kazi ya wanafunzi.

**Zoezi: Majibu**

**Akifisha kifungu hiki.**

Kwa upande wa utunzaji wa utamaduni, mitindo ya Kiafrika ya mavazi inavutia si haba. Mitindo yake ina una rangi mahiri za kupendeza na zenye sifa maarufu. Rangi kama hudhurungi, samawati, kijani na wakati mwingine mchanganyiko wa rangi mbalimbali unavutia macho. Mitindo ya mavazi ya Kiafrika humulika mila na utamaduni wa kabila fulani. Hii hupelekea kuzipa mizizi mila na tamaduni za watu hawa umaarufu usioweza kuondolewa kwa haraka.

## KUANDIKA

1. Mwanafunzi aandike kisa kinalenga madhara ya vita.
2. Mwanafunzi aelezee hatua za dharura atazofuata kumwokoa.
3. Mwanafunzi adhihirishe huduma za kwanza atakazotumia kumwokoa mtoto. Mwalimu ahakiki maelezo.

# SURA YA 5: TEKNOLOJIA

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

**KIFUNGU A**

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kifungu.

**SEKTA YA MAWASILIANO**

**MAJIBU**

1. Sekta ya mawasiliano inasaidia uchumi wa nchi.
2. Bidhaa nyingi huweza kuozea maghalani na hata mashambani kwa sababu ya ukosefu wa magari ya kuzifikisha sokoni kuuzwa.
3. Sehemu zisizo na barabara nzuri hubaki nyuma kimaendeleo.
4. Watu wameweza kujinunulia simu-tamba na Mawasiliano yameimarika.
5. Mashindano ya kampuni za huduma ya mawasiliano yanahimiza zaidi wananchi kuwa na simu.
6. Wasomi wengi wameweza kupata mawazo na maoni mbalimbali kuhusiana na masuala mengi yanaoathiri jamii zao
7. Barua pepe imerahisisha mawasiliano na kuyafanya ya bei nafuu.
8. Mahusiano ya watu yameboreka kupitia kwa mitandao ya kijamii kwa kutengeneza mahusiano mapya kati ya ndugu na marafiki na pia inaongeza mawasiliano kati ya mtu na mtu na hivyo kuboresha mahusiano.
9. Ni mitazamo ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni, kimapenzi, kimichezo.
10. Eleza faida za mitandao ya jamii kwa wafuatao:
    i) Wanafunzi kufanya majadiliano ya kimasomo ,
    ii) Wanaharakati wametumia majukwaa ya mitandao ya kijamii kukutana na kuendesha harakati zao.
    iii) Vyuoni wamekuwa wakiendesha harakati za ufunzaji kupitia mitandao ya kijamii.
11. Mitandao ya kijamii imesaidia watu kupunguza misongo ya mawazo kwa kuwasiliana na watu mbalimbali na kujikuta wamefarijika katika matatizo waliyonayo.
12. Mitandao imewasaidia waliotengeneza fani hiyo kukutana pamoja mtandaoni na hata kuongeza wigo wa kukutana uso kwa uso.

13. Katika mazungumzo kuna kuangalia picha kwenye simu tamba.
14. Vijana wengi wameingia kwenye mitego kwa utoaji mwingi wa taarifa za mtu binafsi. Habari hizi zinaweza kumfanya mtu kuwa muhanga wa mapenzi au kuingizwa katika wizi wa fedha na aina mbalimbali za ujangili mitandaoni. Watu wanatumia taarifa hizo kufanya uhalifu.
15. Utafiti ulionyesha kwamba theluthi mbili ya wafanyakazi hutumia wakati mwingi wa kazi kubadilishana mawazo na watu mitandaoni wakati wa kazi.

**KIFUNGU B**

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kifungu.

**UMUHIMU WA TEKNOLOJIA KATIKA KUFUNZA**

**MAJIBU**

1. Kulingana na aya ya kwanza, mwanafunzi anapata faida gani za vifaa vya teknolojia katika ufunzaji? Wanafunzwa na kuongeza uwezo wao, uzalishaji, na utendaji.
2. Kama una uchovu wa kutoa maelezo ya kinadharia au wanafunzi wako hawawezi kukielewa na kile unachofunza.
3. Dhana ngumu darasani husuluhishwa kwa vifaa vya teknolojia kwa kuifanya dhana wazi kwa kila mwanafunzi katika darasa.
4. Inakusaidia kufuatilia maendeleo ya wanafunzi wako.Kuhifadhi ujumbe na alama za wanafunzi wako kwenye tarakilishi.
5. Kiasi cha karatasi na idadi ya miti itaokolewa ikiwa kila shule iliamua kuanzisha vitabu vya digitali.
6. Wanafunzi watachukua ujumbe kwenye mtandao na kuwasilisha karatasi zao na kazi za nyumbani kupitia barua pepe.
7. Kwa kutumia teknolojia ya skrini ya kugusa na maonyesho ya mtandaoni ili kufanya madarasa zaidi ya maingiliano.
8. Ujifunzaji utampa mwanafunzi nafasi nzuri ya kujiongezea maarifa.

9. Walimu wa shule walikuwa wanafunzi kwa vile walipaswa kutumia saa kadhaa kwenye maktaba ili kutafuta habari waliyohitaji.
10. Hutoa mipangilio ya kipekee kwa wanafunzi kushiriki katika mradi wa kikundi. Wanaweza kufanya kazi kutoka nyumbani; timu inaunganishwa kwa njia ya mtandao na kila mtu anaongozwa na mazingira yaliyo tulivu.
11. 

## SARUFI

### VIVUMISHI

1. Mwalimu awaongoze wamafunzi katika kuzungumzia dhana ya vivumishi katika lugha. Je, kuvumisha ni kufanya nini? Ni maneno yepi katika lugha ya Kiswahili yanaweza kuchukua vivumishi.
2. Kisha, wanafunzi wataje mifano ya vivumishi. Wanaweza kutunga sentensi.
3. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua aina za vivumiishi. Ni vizuri mwalimu akirejelea mifano iliyotungwa na wanafunzi.
4. Wanafunzi watambue aina za vivumishi na kuzingatia kazi yake katika sentensi. Wanafunzi watoe mifano aidi ya kila aina ya vivumishi.
5. Wanafinzi wakamilishe zoezi katika vitabu vyao.
6. Mwalimu ahakiki kazi ya wanafunzi.

### Zoezi

**A. Tunga sentensi ukitumia maneno haya.**

1. maridhawa
2. mwafaka
3. saba
4. bora
5. laini
6. nadhifu
7. shwari
8. dhaifu

Hakiki sentensi za wanafunzi.

**B. Kosoa sentensi zifuatazo.**

1. Msichana hodari alipewa vitabu saba.
2. Kiti duni kilivunjika kwa sababu kilikuwa dhoofu.
3. Maswali sita yalikuwa rahisi sana.
4. Vitafunio rojorojo na laini vililetwa na wageni.
5. Alipanga nguo laini kwenye kabati.

## KUANDIKA

1. Mwanafunzi andike insha juu ya faida za teknolojia.
2. Mwanafunzi ajadili mjadala. Mwalimu hakiki hoja.
3. Mwanafunzi aeleze umuhimu wa teknohama.

# SURA YA 6: AJIRA

## KUSIKILIZA NA KUZUMGUMZA

### KIFUNGU A

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kifungu.

### NJIA ZA KUPATA AJIRA

### MAJIBU

Kuajiriwa au kujiajiri.

1. Kipato kidogo anachopata katika kazi husika, hitaji la kutaka uhuru zaidi binafsi wa kufanya kazi, hitaji la kuweza kutoa ajira kwa wengine, kuweza kutumia vyema kipaji na uwezo wa kuzalisha ambao katika kazi ya sasa mtu hapati nafasi ya kufanya hivyo.
2. Ndoto ya kujiajiri inafanikishwa kwa kuwa na mkakati wa kuifanikisha pamoja na muda hasa wa lini utaitimiza hiyo ndoto.
3. Utafiti kabla ya kujiajiri unahusisha mipango yako binafsi ya maisha, mtazamo wako kuhusu maisha, mpenzi/mke wako, familia yako, na hali ya jamii kwa jumla inavyoenda kama vile mabadiliko ya hali ya kisiasa, teknolojia, na uchumi.
4. Aina ya shughuli unayotaka kuifanya ukiacha kuajiriwa, pima uwezekano wa shughuli hiyo kufanyika kweli, kama itakulipa, aina ya watu na rasilmali nyingine utakazozihitaji na jinsi utakavyozipata.
5. Unahitaji kiasi cha fedha za kutosha kununua vifaa na malighafi ya kutengenezea bidhaa yako, za kuwalipa wafanyakazi wako, za kuendesha maisha yako na familia yako.
6. Hakikisha umetengeneza bajeti ya kutosha na una akiba ya kutimiza mahitaji ya bajeti yako.
7. Utahitaji wateja, washirika, wafanyakazi na hata washauri mbalimbali ili mambo yako yaende vizuri.
8. Ndio wakati muafaka wa kutengeneza na kupanua wigo wako, wa watu unaowafahamu na walio karibu nawe.

9. Kupitia kwa salamu, kuheshimu watu wote, kujenga taswira nzuri kwa jamii kwa lugha fasaha, picha na matukio mengine, kuepuka watu wakufikirie vibaya.

10. Hii itakusaidia kupata uzoefu, kusoma ishara za nyakati, kutambua fursa nyingine zaidi.
11. Jinsi unavyoendelea kujifunza zaidi kuhusu kazi yako, watu na jamii kwa jumla ndivyo unapata ufahamu wa yanayojiri kila wakati.
12. Wafanyikazi wako si watu tu wasiolewa, ni muhimu wawe wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha wa kufanya shughuli husika.
13. Kwa kuwapa nyenzo zote muhimu za kufanyia kazi ikiwemo teknolojia na mazingira mazuri ya kazi.
14. Uvumilivu ni muhimu ili kupata mafanikio kwani hayaji kwa usiku mmoja.

## KUSOMA

**KIFUNGU B**

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kifungu.

### HALI YA AJIRA NA UMUHIMU WA KUJIAJIRI

**MAJIBU**

1. Wasomi, na wasio kuwa wasomi, wenye ujuzi na wasio kuwa na ujuzi wote wamekosa ajira.
2. Aina mbili za sekta ya kuajiri watu ni serikalini na kibinafsi.
3. Bajeti finyu inatajwa kuwa kikwazo.
4. Sekta ya kibinafsi kupitia makampuni, sekta za huduma na ujasiliamari.
5. Ukosefu wa ajira,hali duni ya uchumi wa nchi ,mifumo migumu ya uanzishaji miradi/biashara ya kibinafsi hasa kutoka vyombo vya serikali, elimu itolewayo shuleni na vyuoni,watu wachache wanashikilia uchumi mkubwa wa nchi, mifumo kandamizi na migumu ya kibenki , wasomi wengi wanadharau kazi mbalimbali.

6. Wasio na uwezo hushindwa kufurukuta katika kujiajiri.
7. Sekta ya benki inawakandamizi watu kwa njia za kuwakosesha watu wengi sifa za kuweza kukopa.
8. Wasomi wanachangia tatizo la ukosefu wa ajira kwa vile wengi wanadharau kazi mbalimbali aidha kwa kufikiri tofauti au uzembe tu wa kutojua fursa halisi katika mazingira yao.
9. Vijana wengi huamua kukaa vijiweni, kulala nyumbani, kuzurura mitaani kwa shughuli zisizo na tija, kwa kisingizio cha kusubiri ajira zitangazwe.
10. Eleza dhana ‘kujitolea’ ni kufanya kazi fulani pasi na malipo au malipo duni tu.
11. Kujitolea kunasaidia kujifunza ujuzi mahususi unaohitaji ili kuajiriwa kirahisi bila kulazimika kulipia kwa fedha.
12. Waajiri wengi huweka sharti la waombaji kuonyesha uzoefu wa kazi wanayoiomba kama ushahidi wa uwezo wa kumudu kazi husika.
13. Mtu anayefahamiana na watu wengi kwenye maeneo mbalimbali ya kazi, anajiongezea fursa ya kuunganishwa na taarifa nyingi za kiajira.
14. Hatuishi kwa lengo la kujikusanyia fedha kujiletea faida binafsi na hali ikaishia hapo. Wakati mwingine unaweza kutoa ujuzi, maarifa na nguvu zako kwa lengo tu la kuhisi furaha ya kutoa mchango wako katika kuboresha maisha ya wengine.
15. Maana zipo taasisi za kinyonyaji zinazopenda kutumia nguvu za watu bure.

**KIFUNGU C**

Kabla ya kujibu maswali ya kifungu, wanafunzi wakisome kwa makini huku wakizingatia matamshi bora. Mwalimu akosoe matamshi yoyote yale. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika kifungu.

**WASIFUKAZI**

## MAJIBU

1. Wale wanaopaswa kuandika wasifu kazi ni watafuta ajira na hata wenye ajira tayari.

2. Wasifu kazi husaidia kuonyesha uwezo na ubora wako wa kitaaluma na katika utendakazi wa mtu.
3. Athari ya tawasifu yenye makosa ni kukosa ushawishi na pengine kupuuzwa na waajira hasa kwa wale wanaotafuta ajira.
4. Makosa ya kimaandishi katika tawasifu yanaweza kutokea kwa njia mbili kwa sababu ya ukosefu wa makini au kutojidhihirisha baada ya kuandaa wasifu.
5. Njia mbili za kuhakikisha wasifu kazi wako hauna makosa ya kimaandishi ni kupitia mara kadhaa na kujidhihirisha kama hakuna makosa yoyote ya kiuandishi, pia kumpa mtu mwingine akusaidie kupitia.
6. Maana ya uandishi usiowiana wa tawasifu ni kuwa na mtindo na ukubwa wa maandishi yasiyolingana.
7. Vichwa katika wasifukazi vinapoandikwa vinatakiwa kuwa sawa.
8. Rangi inayopendekezwa kwa maandishi ya wasifukazi ni nyeusi.
9. Vitu viwili vinavyoweza kukosesha mtu kazi akiviweka katika wasifukazi wake ikiwa haujaambiwa kufanya hivyo ni imani ya dini yako na picha yako.
10. Kama unaomba ajira kwenye shirika la dini na unahisi kutaja dini yako kutakuongezea nafasi ya kuchaguliwa
11. Hakikisha kuwa wasifu wako unakidhi mahitaji ya kazi husika.
12. Katika urefu wa wasifukazi zingatia vitu vya msingi vya kuweka kwenye wasifu wako na kuviweka katika mpangilio mzuri.
13. Alama ulizopata kwa kila somo ulipokuwa chuoni.
14. Ni sehemu ya uzoefu.
15. Madhara ya kutosema ukweli katika wasifukazi ni kuwa kunaweza kukufanya uonekane mtu ambaye si mwaminifu na hivyo kuharibu sifa yako.

## SARUFI

### VIAMBISHI

1. Mwalimu arejelee nyakati ambazo wanafunzi wametumia viambishi kama vile vya nyakati na hali.

2. Nwalimu awajumuishe wanafunzi katika kuzungumzia dhana ya viambishi.
3. Wanafunzi waweze kutambua aina mbili kuu za viambishi: viambisha awali na viambishi tamati.
4. Wanafunzi waelezee viambishi hivi hupatikana wapi katika kitenzi.
5. Wanafunzi wataje baadhi ya mambo yanayotajwa na matumizi ya viambishi awali na viambiahi tamati.
6. Mwanafunzi wakamilishe zoezi katika vitabu vyao.
7. Mwalimu ahakiki kazi ya wanafunzi.

## Zoezi

**Onyesha viambishi mbalimbali katika maneno yafuatayo.**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | yanayotumiwa - | ya-na-yo-tum-iw-a |
| 2. | unachoona- | u-na-cho-on-a |
| 3. | imesimuliwa | i-me-simul-iw-a |
| 4. | ulimwangukia | u-li-mw-anguk-i-a |
| 5. | alifanyishwa | a-li-fany-ish-w-a |
| 6. | atakapovuna | a-ta-ka-po-vun-a |
| 7. | umenunuliwa | u-me-nunu-liw-a |
| 8. | huchelewa | hu-chelew-a |
| 9. | nimekuuliza | ni-me-ku-uliz-a |
| 10. | nendeni | ne-nd-e-ni |

## KUANDIKA

1. Mwanafunzi andike wasifukazi wa kutafuta kazi. Mwalimu ahakiki kazi ya mwanafunzi.
2. Mwanafunzi aJadili mswada kwa maoni yake.
3. Mwanafunzi ajadili changamoto za kujiajiri. Mwalimu ahakiki hoja.